TANGAZO LA SERIKALI Na.683 la tarehe 13/9/2019

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA YA 290

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya vifungu vya 7(1) (u) na 16 (1)*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA NANYUMBU ZA MWAKA, 2019

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu za Mwaka, 2019

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi, zitatumika katika eneo lote la Halmashauri Wilaya ya Nanyumbu.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi yeyote wa Halmashauri au mtu yeyote mwingine atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu.

"hesabu" maana yake ni jumla ya mauzo au ununuzi ikiwa ni pamoja na ushuru na ada katika mwaka husika wa mapato.

"hesabu za mwisho" maana yake ni taarifa za kihasibu zinazowasilishwa na mlipa ushuru baada ya kipindi cha hesabu kwa mujibu wa kifungu cha 13 cha Sheria Ndogo hizi, zikijumuisha nyaraka, hesabu au maelezo yoyote yahusuyo kiasi na

thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizowasilishwa, kusambazwa, kutolewa au kuuzwa kibiashara;

"kipindi cha hesabu" maana yake ni muda ambao mlipa ushuru itatakiwa kuwasilisha hesabu za mauzo yake;

'Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu au mtumishi yeyote atakayeteuliwa kwa wakati huo kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mlipa ushuru" maana yake ni kampuni, tawi la kampuni, mtu au taasisi inayofanya biashara katika eneo la Halmashauri;

Sura ya 290

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa.

"Ushuru wa Huduma" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kutoka kwa kampuni, tawi la kampuni, mtu au taasisi inayofanya biashara yenye leseni iliyotolewa chini ya Sheria yoyote kwa huduma za umma inazotumia kufanya biashara katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni mtu, kikundi cha watu au kampuni iliyoingia mkataba na Halmashauri kwa ajili ya kukusanya ushuru wa huduma.

Utozaji wa Ushuru

4. (1) Halmashauri itatoza na kukusanya Ushuru wa huduma kutoka kwa kila mlipa ushuru.

(2) Ushuru utakaotozwa kwa mujibu wa Kifungu kidogo cha (1) utatozwa katika kila kipindi cha hesabu kwa kiwango cha asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya mauzo ya bidhaa au huduma yanayofanyika katika eneo la Halmashauri baada ya kutoa Kodi

ya Ongezeko la Thamani na Ushuru wa Bidhaa.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 4 cha Sheria Ndogo hizi mfanyabiashara ambaye hawasilishi hesabu zake mamlaka ya Mapato Tanzania atalipa Ushuru wa Huduma kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

Ukaguzi wa kumbukumbu za biashara

5. Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala anaweza katika muda wa kazi, kuingia kwenye jengo au eneo la biashara la mlipa ushuru kwa nia ya kufanya ukaguzi na tathmini ya kumbukumbu za biashara, vitabu vya hesabu na taarifa nyinginezo kama atakavyoona inafaa kufanyiwa ukaguzi kwa ajili ya kujua kiwango sahihi cha ushuru kinachotakiwa kulipwa.

Taarifa kwa mlipa Ushuru

6. (1) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Mkurugenzi anaweza kwa taarifa ya maandishi ya siku saba, kumtaka mlipa ushuru kuwasilisha kumbukumbu za kibiashara na vitabu vya hesabu, kwa nia ya kupata taarifa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini au kukusanya Ushuru wa Huduma.

(2) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa masharti ya kifungu kidogo cha (1), Mkurugenzi anaweza kumtaka mlipa ushuru kufika mbele yake.

Muda wa Kulipa

7. Bila kuathiri masharti ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa na sheria nyingine yoyote, kila mlipa ushuru atatakiwa kuwasilisha hesabu za awali na kulipa ushuru unaotakiwa katika kila kipindi cha miezi mitatu katika mwaka wa fedha wa Serikali.-

Hesabu za mwisho

8. (1) Kila mlipa ushuru atatakiwa kuwasilisha kwa Halmashauri hesabu za mwisho katika kipindi cha miezi mitatu tangu kumalizika

kwa kipindi cha hesabu.

(2) Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa anaweza:
- (a) kukubali hesabu za mwisho na kutathmini ushuru katika msingi huo;
- (b) kukataa hesabu za mwisho na kufanya tathmini kuhusu hesabu hizo iwapo atakuwa na sababu za msingi za kuamini kuwa hesabu hizo siyo sahihi.

(3) Iwapo mlipa ushuru hajawasilisha hesabu za mwisho kwa mwaka wa fedha husika na ametakiwa kufanya hivyo kwa notisi ya siku thelathini (30), Mkurugenzi anaweza kwa kadri atakavyo ona inafaa, kuamua kiwango cha hesabu za mlipa ushuru huyo, kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(4) Ushuru uliothaminiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, utalipwa katika siku thelathini (30) tangu tarehe ya kufanya tathmini.

Makosa na Adhabu

9. (1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:-

- (a) ndani ya muda ulioainishwa katika Sheria Ndogo hizi;
- (b) atashindwa kuwasilisha hesabu sahihi kwa Halmashauri;
- (c) atashindwa kutunza kumbukumbu yoyote au nyaraka kwa ajili ya ukaguzi;
- (d) atamzuia au atajaribu kumzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake aliyopewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Mtu yeyote atakayetiwa hatiani kwa kosa lililoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi Milioni moja (1,000,000/=) au kutumikia kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au adhabu zote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Mamlaka ya Mkurugenzi kufifilisha kosa

10. (1) Bila ya kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hizi, Mkurugenzi atakuwa na mamlaka ya kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote atakayekiri kutenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi na kuwa tayari kulipa Ushuru wa Huduma, kiasi cha fedha kisichozidi shilingi laki tano (500,000/=).

(2) Mtu atakayekiri kosa chini ya kifungu kidogo cha (1) atatakiwa kujaza fomu maalum iliyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

## JEDWALI LA KWANZA

Limetungwa chini ya kifungu cha 4(3)

| Na | Aina ya Biashara | Kiwango | Muda |
|---|---|---|---|
| 1. | Saloon | 20,000/= | Mwaka 1 |
| 2. | Gereji na karakana | 20,000/= | Mwaka 1 |
| 3. | Duka la jumla | 20,000/= | Mwaka 1 |
| 4. | Duka la rejareja | 20,000/= | Mwaka 1 |
| 5. | Bucha | 20,000/= | Mwaka 1 |
| 6. | Bar | 20,000/= | Mwaka 1 |
| 7. | Grosary | 20,000/= | Mwaka 1 |
| 8. | Biashara na huduma nyinngine | 20,000/= | Mwaka 1 |

JEDWALI la pili

***(Limetungwa Chini ya Kifungu cha 10 (2))***

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………………. mwenye Simu Na.…………………….. wa S.L.P……………..ninayefanya biashara……………………………….. katika eneo la ……………………….. lililopo katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu, kwa hiari yangu mwenyewe nakiri kuwa tarehe………mwezi………… mwaka…………. nilikiuka kifungu cha………… cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu za mwaka 2019.

Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushurutishwa na mtu yeyote nakubali kulipa faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi ataamua kutekeleza madaraka yake aliyopewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Jina…………………………………………………………………….

Saini:…………………………… Tarehe: ……………………………

MBELE YANGU**:**

Jina:……………………………………………………………………

Saini:…………………………………………………………………..

Wadhifa:………………………………………………………………

Tarehe:…………………………………………………………………

Tangazo La Serikali Na. 683 (linaendelea)

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu iligongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 28/4/2018 na iligongwa mbele ya:-

PONSIAN KAZEE
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya
Nanyumbu

L.S

AHMAD B. MCHOPA
Mwenyekiti
Halmashauri ya Wilaya
Nanyumbu

NAKUBALI

SELEMAN S JAFO (MB.
Waziri wan chi OR Tamisemi

Dodoma
Tarehe 14 Agosti, 2018